

Jarida la Wizara ya Afya

Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 11, SEPTEMBA 2023



TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO



BODI YA UHARIRI

MWENYEKITI
Dkt. John Jingu
KATIBU MKUU

MHARIRI
Englibert Kayombo

MHARIRI MSAIDIZI
Emmanuel Malegi

WAJUMBE
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaiza
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga

WASANIFU
Englibert Kayombo
Said Nyaiza



@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

YALIYOMO

Rais Samia azindua Hospitali ya Kanda Kusinil...UK 1



Uwekezaji uliyofanyika uen-dane na ubora wa huduma Hospitali ya Kanda Kusini - Mtwara.... UK 2

Rais Samia afanya miujiza Sekta ya Afya UK 3



Dkt. Jingu ataka mpango mkakati madhubuti wa utoaji huduma za Afya na chachu ya ukuaji wa uchumi..... UK 4

Tumieni taaluma zenu kuwaelimi-sha wananchi kuhusu Polio UK 6



US - CDC yaahidi kuendelea kushirikiana na tanzania katika kuimarisha huduma za afya.... UK 7

Moi yapokea vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi Bilioni 3 kutoka uingereza.... UK 8



**Tanzania kushirikiana na Marekani
kuboresha mifumo ya usimamizi
masuala ya afya.... UK 9**



**Waziri Ummy asisitiza matumizi
sahihi ya ARV kwa wenyewe VVU.... UK
20**



**Huduma za CT Scan kuwanufaisha
wananchi wa Lindi na nchi jirani
.... UK 10**

**Tanzania na Afrika Kusini zasaini
makubaliano ya ushirikiano
katika sekta ya afya UK 12**



**Watoto zaidi ya milioni 3 kupata
chanjo ya Polio kwenye mikoa 6
nchini.i UK 21**



**“Utaratibu wa Bima ya afya ni
kuchangiana sio lazima
mpaka uugue” – Dkt. Mollel... UK 13**



**Bima ya Afya kwa wote suluhu ya
kudumu ya matibabu kwa rika
zote UK 22**

**Rasilimali zaidi zinahitajika
kupambana na ugonjwa wa
Malaria UK 16**



**Watoa huduam 5,291 kutoa
chanjo ya Polioo.... UK 23**



**Tanzania yahimiza usawa katika
kukabiliana na Majanga UK 17**



**Wataalamu wa kutibu Saratani
watakiwa kujikita katika kufanya
tafiti UK 24**

**Vifaa vya kujipima UKIMWI Milioni
1.6 vimesambazwa Nchini 18**



**Endeleeni kumsaidia Dkt. Samia
kulinda afya za watanzania - Mhe.
Nyongo.... UK 25**



**Wataalamu wa magonjwa ya ini
afrika wakutana katika kongamano
tanzania.... UK 19**



**Tunduma
yapongezwa kwa
kuajiri watumishi
wa afya wa
mkataba.... UK 26**

Rais Samia azindua Hospitali ya Kanda Kusini, asisitiza utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi na kwa lugha nzuri.

**Na. Majid Abdulkarim,
Mtwara**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mapema leo hii Septemba 15, 2023 amezindua Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara.

Rais Samia amesema kuwa kukamilika kwa Hospitali hiyo ambayo ina watalaam, vifaa na vifaatiba vyta kisasa itasaidia watu wa Kanda ya Kusini inayojumuisha Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma kupata uhakika wa huduma za matibabu ya kibingwa karibu na maeneo yao.

"Wagonjwa wote wenye matatizo makubwa watakuja hapa, jengo hili litumike kutoa huduma za afya" amesema Rais Samia.

Rais Samia amesema kuwa kazi ya watumishi wa afya ni kuokoa maisha ya watu hivyo watumishi hao wajitumie kufanya kazi kwa kuwa Serikali imewekeza kwenye miundombinu, vifaa na dawa na wao watimize wajibu wao

Tunahitaji matunzo ya jengo hili, vifaa na huduma kwa wananchi kwa lugha nzuri, kila mtu amepangiwa jukumu lake na Mwenyezi Mungu, tumridhishe Mungu kwa huduma tunazozitoa, nawatakia kila la kheri" amesema Rais Samia huku akiongezea kuwa chagamoto zilizopo za watumishi zitaendelea kufanyiwa kazi kwa haraka.



Uwekezaji uliyofanyika uendane na ubora wa huduma Hospitali ya Kanda Kusini - Mtwara



Na Hassan Kimweri Mtwara

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amewataka watumishi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini kuhakikisha kuwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Samia Suluh Hassan katika Hospitali hiyo ikiwemo ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa, kuajiri watumishi pamoja na uhakika wa upatikanaji wa dawa unaendana na ubora wa huduma zinazotolewa kwa wananchi.

Waziri Ummy ametoa wito huo leo Septemba 15,2023 wakati akizungumza na Watumishi wa Afya katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kufungua Hospitali hiyo

Aidha Mhe. Ummy amewapongeza watumishi kwa huduma bora zinazotolewa huku akiwasitiza kufanya kazi kwa kuzingatia weledi, maadili na viapo vya Taaluma zao.

“Niwapongeze sana kwa huduma bora mnazozitoa, hospitali hii ina jengo zuri sana, vifaa tiba kwaiyo kilichobaki ni ubora wa huduma”. Ameeleza Waziri Ummy

Mhe. Ummy Mwalimu amewahakikisha watumishi wa hospitali hiyo kuapatia gari aina ya Coaster moja kwa ajili ya kuwarahisishia kufika kazini. “Tutaleta angalau gari moja ili kuwarahisishia watumishi kufika kwa wakati eneo la kutolea huduma”, amesitiza Waziri Ummy.

Waziri Ummy amesema kuwa ataendelea kuwa balozi wao kwa kuwasema, kuwalinda, pamoja na kuwatekelezea stahiki zao lakini kila mtumishi atimize wajibu wake ili kuleta ubora wa Huduma kwa wananchi wanao wahudumia.





Rais Samia afanya miujiza Sekta ya Afya

**Na. Majid Abdulkarim
Mtwara**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya miujiza katika sekta ya afya kwa kutoa zaidi ya shilingi Bilioni 24 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara.

Kauli hiyo imebainishwa leo Mkoani Mtarawa na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel wakati akitoa salamu katika Mkutano wa Hadhara wa Rais Samia na Wananchi wa mkoa wa Mtwara.

Dkt. Mollel asema kuwa Rais samia amezindua Huduma katika hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara ikiwepo mashine ya CT Scan na X Ray tatu ambazo zote hizo zina Ghali mu Bilioni 7.5 ya vifaa vyote vilivyopelekwa katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara

Aidha amesema kuwa Rais samia amehakikisha fedha zote za dawa zinatoka kwa asilimia 100 na sasa umetoa Bilioni 17 kwa ajili ya ujenzi wa Bohari ya Dawa kanda ya kusini na ujenzi umeanza

Ameeleza kuwa Raisd Samia kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwa mkoa wa Mtwara kwenye sekta ya afya ameleta Bilioni 22 na katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara kuna ujenzi unaendelea unaoghalimu Bilioni 9.3 na ujenzi umefikia asilimia 88 na kwa mantiki hiyo wanamtware wamepata hospitali ya kisasa itakayowapa Huduma zote katika mkoa huo

"Mhe. Rais mpaka sasa Mkoa wa Mtwara una CT Scan mbili moja katika hospitali ya Rufaa ya Kanda na nyingine katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara ili moja ikipata changamoto nyingine inaendelea kutoa Huduma kwa wananchi wa ukanda wa kusini", ameela-za Dkt. Mollel

Ameongeza kuwa kwa miaka miwili ya Rais Samia katika sekta ya afya ametoa Tiloni 6.7 ambayo imefanya mapinduzi makubwa katika sekta ya afya nchini kwa kununua CT Scan 32, X Ray za kisasa 199 na kufanya nchi kuwa na jumla ya X Ray 543.

"Hivyo kwa mtu aliyeko Tandahimba, Newala akipata Huduma ya X Ray tunauwezo wa kuunganisha na kusoma majibu yake kwa kutumia X Ray za kisasa zilizo simikwa katika hospitali zetu chini ya uongozi imara wa Rais Samia", Ameelzea Dkt. Mollel

Vile vile amemponeza Rais Samia kwa kukabidhi magari matatu na moja wapo ya gari hilo linaubora wa kutoa huduma kwa mgonjwa maututi (ICU).





Dkt. Jingu ataka mpango mkakati madhubuti wa utoaji huduma za Afya na chachu ya ukuaji wa uchumi

Na Emmanuel Malegi
Dodoma

Katibu Mkuu wa Wizara ya afya Dkt. John Jingu amewataka wataalam wa afya kuandaa mpango mkakati madhubuti utakaokua ni muongozo katika kutoa huduma za afya nchini na kuwafikia wananchi popote walipo ikiwemo kuangalia fursa za kiuchumi ndani na nje ya nchi.

Dkt. Jingu amesema hayo leo wakati akifungua kikao cha Wataalam mbalimbali wa afya waliokutana jijini Dodoma kwa ajili ya kuandaa mpango wa Wizara ya Afya wa kuboresha utoaji wa huduma za nchini.

Dkt. Jingu amesema Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na taasisi binafsi imewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya na anategemea uwekezaji huo ulete matokeo Chanya kwa nchi hivyo wataalam wanatakiwa kuchangamkia masoko ya ndani na nje.

"Rais Samia Suluhu Hassan anataka sekta ya afya ikue Tanzania na kutoa mchango mkubwa kuliko hivi sasa, haya yote yanawezekana kwa kuweka sera na miongozo mizuri lakini kutoa huduma kupitia taasisi zetu mbalimbali za umma na za sekta binafsi".

Amesema Dkt. Jingu.

Dkt. Jingu ameongeza kuwa sekta ya afya kazi yake sio kutoa huduma peke yake kwa wagonjwa au kuzuia na kupambana na magonjwa bali inatakiwa iwe chanzo cha ukuaji wa uchumi wa nchi hivyo amewataka wataalam hao kuweka mikakati itayofungua fursa za kiuchumi kupitia afua mbalimbali za afya.

"Mwelekeo wa Rais ni kuona huduma za afya hapa nchini zinakua ni nzuri lakini bidhaa za afya zikiwemo dawa, vifaa na vifaa tiba vinapati-kana muda wote kwa urahisi na kwa bei ambayo mwananchi wa kawaida anaweza kuimudu lakini pia muangalie vikwazo vinyovkamisha fursa na muweke mikakati ya kutoa vikwazo hivyo ili nchi ipate masoko ya nje". Amesema Dkt. Jingu.

Aidha, Dkt. Jingu amesema kuna fursa nyingi katika ukanda wa Afrika Mashariki, kusini mwa jangwa la sahara, Afrika na duniani kwa ujumla kuhusu masuala ya afya akitolea mfano mkataba wa Jumuiya ya maendeleo kusini mwa Afrika (SADC) na Bohari ya Dawa (MSD) kuhusu kununua, kuuza na kusambaza bidhaa za dawa kwenye nchi wanachama wa jumuiya hiyo kuwa ni mojawapo ya fursa ya kiuchumi Tanzania inayonufaika nayo.

Tuweke mifumo mizuri ya muunganiko kati ya Wizara ya Afya na TAMISEMI

Na. Shaban Juma

Dodoma

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe amesitiza umuhimu wa kuweka mfumo wa muunganiko kati ya Wizara ya Afya na TAMISEMI ili kuwa na muunganiko mzuri wa kujua idadi ya watumishi pamoja vifaa tiba.

Dkt. Magembe ameyasema hayo Septemba 7,2023 wakati wa mkuato wa kitengo cha huduma za uchunguzi wa magonjwa ukiendelea pamoja na wadau wa huduma za uchunguzi wa magonjwa uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.

“Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI kwakweli tunahitaji kuweka mfumo mzuri wa muunganiko kati ya Wizara ya Afya na TAMISEMI ili kuwa na muunganiko mzuri wa kujua idadi ya watumishi pamoja vifaa tiba”. Amesema Dkt. Magembe

Aidha, Dkt Magembe amewaomba wadau hao kuendelea kusaidia kuimarisha mifumo yetu inayoweza kutambua baina ya wizara ya afya na TAMISEMI ili fedha zinazopatikana ziweze kutumika kwa ufanisi na kutatua changamoto za uchunguzi wa Afya kwa wananchi.

“Kwakweli wadau wetu tunawaomba muendelee kusaidia katika kuimarisha mifumo hii ili tuweze kujua na kuona fedha zinapopatikana lakini pia tujue namna zinavyotumika katika kutatua changamoto za wananchi”. Amesema Dkt. Magembe

Vilevile Dkt. Magembe amesema uchunguzi wa kisayansi ni taaluma inayohitaji ushirikiano wa karibu hivyo wadau wa huduma za uchunguzi wa magonjwa na kitengo cha huduma za uchunguzi

wa magonjwa wanapaswa kukaa pamoja ili kuelewa nani anahitaji msaada na jinsi ya kushirikiana katika kutumia data nyingi zinazozaliswa.

Pia, amesema kuwa ni muhimu sana kuimarisha huduma za uchunguzi, haswa kuanzia ngazi ya Msingi, tunawaomba wadau wote kuwa na mtazamo wa Kisekta na kuwa wataalam ili iwezekane kuoatikana kwa majibu sahihi na kuepuka kuwachanganya wananchi.

“Tunaona kuna umuhimu mkubwa kwa wadau wetu kuanza na mtazamo wa Kisekta kuanzia ngazi ya msingi kwakuwa wananchi ndipo wanapoanza kupata huduma hadi ngazi ya juu kwa kuimarisha huduma za uchunguzi”. Amesema Dkt. Magembe





Tumieni taaluma zenu kuwaelimisha wananchi kuhusu Polio

**Na Shaban Juma,
Songwe**

Mganga mkuu wa serikali Prof. Tumaini Nagu amewataka watumishi wa Afya kutumia weledi wa taaluma yao katika kutoa elimu dhidi ya magonjwa mbalimbali kwa wananchi ili kuendelea kutoa huduma bora za afya.

Prof. Nagu amesema hayo akiwa ziarani mkoani Rukwa akikagua utoaji wa huduma katika vituo vya Afya na zahanati kwa ajili ya maandalizi ya uchanjaji wa Polio itakayoanza tarehe 21-24 septemba 2023.

Aidha, Prof. Nagu amesisitiza uwajibikaji kwa watumishi hao ikiwa ni pamoja na kuzingatia maadili ya taaluma zao ili kuisaidia serikali katika kutoa huduma bora.

“Niwasilitize watumishi wenzangu, maadili kwenye kazi ndio msingi wa utoaji huduma, Huduma ye yeyote anayopata mgonjwa na matokeo yake ni siri katika ya mgonjwa na daktari”. Amesisitiza Prof. Nagu.

Hata hivyo Prof. Nagu amewapongeza watumishi wa Zahanati ya Kilimahewa katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa juhudini wanazozionyesha katika kuwashudumia wananchi ikiwa ni pamoja na kumgundua mtoto wenye virusi vya Polio.

“Niwapongeze watumishi wote wa hapa kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kujitoa na kuwashudumia wananchi, niwaombe tuendelee kutoa huduma bora ili tuimarishe afya za wananchi”. Amesema Prof. Nagu.

Prof. Tumaini Nagu amewasili mkoani Rukwa kwa ziara yake ya siku mbili kwa ajili ya kukagua huduma zitolewazo katika vituo vya Afya, zahanati na kuangalia maandalizi ya Kampeni ya Uchanjaji wa Polio.



US - CDC yaahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuimarisha huduma za afya

**Na. Englibert Kayombo,
Atlanta, USA.**

Taasisi ya kukinga na kudhibiti Magonjwa ya Marekani (US - CDC) imeahidi kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuimarisha huduma za Afya ya Jamii.

Hayo yamebainishwa Jana Septemba 26, 2023 na Mkurugenzi wa masuala ya Afya ya kimataifa wa US - CDC Dkt. Howard Zucker wakati wa ziara ya Waziri wa Afya Tanzaniza Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) na Waziri wa Afya wa Zanzibar Mhe. Nassor Mazrui (Mb) walipoitembelea Taasisi hiyo.

Aidha, Waziri Ummy amesema yeye pamoja na Waziri Mazrui na timu waliyoambatana nayo wametembekea Taasisi hiyo kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika uendeshaji wa mifumo ya kuzuia na kukabiliana na magonjwa katika jamii pamoja na kujifunza uundwaji na uendeshaji wa Taasisi ya Taifa ya Afya ya Jamii.

"Tumefanya mazungumzo na viongozi wa juu wa Taasisi hii ya US - CDC wakiongozo-wa na Mkurugenzi wa masuala ya Afya ya Kimataifa wa US - CDC Dkt. Howard Zucker ambapo ameipongeza sana Serikali ya Tanzania kwa uongozi imara katika kuboresha huduma za Afya ya jamii". Amesema Waziri Ummy

Pia, Taasisi ya US - CDC imetoa tuzo za kutambua michango ya Mhe. Ummy na Mhe. Mazrui katika kutambua usimamizi thabiti na wenyе matokeo katika kudhibiti janga la UVIKO - 19.

Sambamba na hilo, Waziri Ummy alimshukuru Mkurugenzi Mkazi wa CDC nchini Tanzania Dkt. Mahesh Swaminathan kwa kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa vipaumbele vya Serikali hususani katika kupambana na magonjwa ya UKIMWI na Kifua Kikuu pamoja na masuala ya usalama wa Afya ya Kimataifa.

"Lakini pia naishukuru na kuipongeza sana US - CDC kwa kutoa msaada wa kitaalam na rasilimali fedha zilizowezesha kudhibiti ugonjwa wa Virusi vya Marburg uliotokea nchini Tanzania na kufanikiwa kuimaliza mlipuko huo ndani ya muda mfupi". Amesema Waziri Ummy

Viongozi hao walikubaliana kuendelea kushirikiana katika kuimarisha uratibu wa magonjwa ya Afya ya jamii na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ambapo US - CDC waliahidi kutoa msaada wa kitaalam na rasilimali fedha zitakazowezesha kuanzisha Taasisi ya Taifa ya Afya ya Jamii nchini Tanzania.



Moi yapokea vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi Bilion 3 kutoka Uingereza

Na. Cletus Sanga

Dar es salaam

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu kwa niaba ya Waziri Mhe. Ummy Mwalimu amepokea msaada wa vifaa tiba vyenye upasuaji kutoka Jumuiya ya St. Roch ya nchini Uingereza wenye thamani ya shilingi bilioni 3.

Dkt. Jingu amepokea vifaa hivyo wakati alipotembelea Taasisi ya Mifupa ya MOI Katika hafla fupi ya makabidhiano na uzinduzi wa kambi ya siku nane ya matibabu iliyofanyika leo Septemba 21, 2023 katika Ukumbi wa MOI jijini Dar es Salaam.

Dkt. Jingu ameishukuru Jumuiya ya St. Roch na Madaktari hao kwa msaada wa vifaa tiba na kuongeza kuwa utasaidia kuboresha huduma kwenye taasisi hiyo.

Amesema vifaa hivyo vitatumika katika upasuaji wa kubadilisha nyonga na magoti, urekebishaji wa misuli ya magoti kwa njia ya matundu, urekebishaji wa ulemavu kwa watoto na upasuaji wa tishu (soft tissue surgery) pamoja na huduma nyingine za kibingwa.

"Msaada mlioutoa ni mkubwa sana, amesema Mkurugenzi Mtendaji wa MOI Prof. Abel Makubi ameishukuru Jumuiya ya St. Roch ya nchini Uingereza kwa msaada wa vifaa tiba vyenye upasuaji na kwamba vifaa na ujio wao utaleta matokeo chanya kwa MOI.

upasuaji hapa MOI". Alisema Dkt. Jingu.

Akizungumzia kambi ya matibabu Katibu Mkuu huyo alisema itasaidia kukuza ujuzi kwa madaktari wazawa na kwamba fursa hiyo italeta matokeo chanya katika utoaji tiba kwa wananchi.

"MOI hii baada ya siku nane, wageni waki-ondoka haitakuwa MOI hii, kutakuwa na mabadiliko makubwa sana, hii ni fursa ya kila mmoja kujifunza, fursa hii itatoa matunda chanya na ya kudumu kwa jamii yetu". Alisema Jingu.

"MOI ni kituo cha umahiri sio tu kwa Tanzania lakini pia katika ukanda huu, unaenda kuimarisha pia ushirikiano baina ya Tanzania na Uingereza, matarajio yangu kwamba ushirikiano huu baina ya Taasisi yetu ya MOI na Jumuiya ya madaktari bingwa wa mifupa kutoka Uingereza utakuwa endelevu na wenye tija kawa manufaa ya watanzania wote". Ameongeza Dkt Jingu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MOI Prof. Abel Makubi ameishukuru Jumuiya ya St. Roch ya nchini Uingereza kwa msaada wa vifaa tiba vyenye upasuaji na kwamba vifaa na ujio wao utaleta matokeo chanya kwa MOI.

Tanzania kushirikiana na Marekani kuboresha mifumo ya usimamizi masuala ya afya



**Na. Englibert Kayombo,
Washington USA.**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeingia makubaliano na Serikali ya Marekani juu ya uboreshaji wa mifumo ya usimamizi wa masuala ya Afya kwa kwa kuanzisha Maabara za Taifa za Afya ya Jamii za kisasa.

Makubaliano hayo yamefikiwa mara baada ya Waziri wa Afya Tanzania Mhe. Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya Zanzibar Mhe. Nassor Mazrui kufanya kikao na Mkuu wa Masuala ya Kimaita Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu nchini Marekani Bi Susan Kim, kwa kujadiliana kuhusu uboreshaji wa mifumo ya usimamizi wa masuala ya Afya.

“Tumekuja hapa kujifunza jinsi idara hiyo inavyosimamia na kuratibu huduma za maabara za Kitaifa za Afya ya Jamii ambapo tumekubaliana kuanzisha Maabara za Taifa za Afya ya Jamii ambazo zitakuwa na jukumu la ufuatiliaji wa magonjwa hususani yanayoathiri afya ya jamii na vihatarishi vyake, uchunguzi wa magonjwa na tafiti za masuala ya afya ya jamii” amesema Waziri Ummy Mwalimu

Amesema, uanzishwaji wa maabara hizo utaimarisha uwezo wa Tanzania katika kujikinga, kijiandaa na kukabiliana na majanga ya afya kama vile UVIKO 19, Marburg na Ebola





Huduma za CT Scan kuwanufaisha wananchi wa Lindi na nchi jirani

**Na. Majid Abdulkarim
Lindi**

Huduma za CT-Scan katika Mkoa wa Lindi zinakwenda kupunguza adha ya wananchi kusafiri kwa umbari mrefu kufuata huduma hizo Mikoa ya jirani.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel kwa niaba ya Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu katika Mkutano wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan na wananchi wa Mkoa Lindi katika viwanja vya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa huo.

Dkt. Mollel amesema kuwa faida za kuwa na huduma ya CT-Scan Mkoani humo imeishaonekana ambapo mpaka sasa zaidi ya watu 108 wamepata huduma hiyo katika Hospitali hiyo ambao walitakiwa kusafiri kwenda Mikoa ya jirani.

Sambamba na hilo Dkt. Mollel amesema kuwa jengo la wagonjwa wa dharura pia limekamilika na tayari vifaa vimeshasimikwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wa Mkoa huo pamoja na nchi za jirani.

"Mhe Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa niaba ya Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu tunakushuru sana kwa uwekezaji mkubwa ulioufanya katika Sekta ya Afya hapa nchini mpaka sasa nchi jirani wanakuja kupata huduma za Afya Tanzania". Amesema Dkt. Mollel.





Watumishi watakiwa kutunza vifaa vya huduma

**Na. Majid Abdulkarim
Lindi**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan amewataka watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi kutunza vifaa vya kutolea huduma za afya kwa wananchi kwani vimeigharimu Serikali fedha nyingi.

Rais Samia amesema hayo leo tarehe 19 Septemba 2023 wakati akiweka jiwe la msingi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi.

Hospitali hiyo imegharimu shilingi Bilioni 4.8 katika ujenzi wake pamoja na ununuvi wa Vifaa na tayari mpaka sasa imeshatoa huduma ya CT Scan kwa wananchi 108.

Aidha, uwekaji wa jiwe la msingi katika Hospitali hiyo umeenda sambamba na utoaji wa huduma za wagonjwa wa nje

(OPD), Huduma za wagonjwa wa dharura (EMD), huduma za Radiolojia pamoja na huduma za CT Scan hivyo kuwaondolea kero wananchi wa mkoa huo kusafiri mwendo mrefu kufuata huduma hizo.



Tanzania na Afrika Kusini zasaini makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya afya

Johannesburg,
Afrika ya Kusini

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Afrika Kusini zimeingia makubaliano ya ushirikiano katika Sekta ya Afya baina ya nchi hizo mbili ili kuweza kuboresha zaidi huduma za afya na ushirikiano wa pamoja katika kubadilishana uzoefu na watalaam wa Afya.

Makubaliano hayo yamefanya Septemba 1, 2023 kupitia Waziri wa Afya Tanzania Mhe. Ummy Mwalimu na Waziri wa Afya Afrika Kusini Mhe. Dkt. Mathume Joseph Phaahla Jijini Johannesburg, Afrika Kusini na kushuhudwa na Balozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini, Mhe Gaudence Salim Milanzi.

"Tanzania na Afrika Kusini zimekuwa na ushirikiano wa

muda katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya Afya, kusainiwa kwa hati hii kutachangia kuboresha ushirikiano katika sekta ya Afya ikiwemo kubadilishana wataalam wabobezi kwenye fani mbalimbali za afya, kuwezesha mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu na kubadilishana teknolojia, kuboresha upatikanaji wa dawa, chanjo na udhibiti wa magonjwa ya mlipuko pamoja na dharura za Afya" Amesema Waziri Ummy na kuongeza kuwa ushirikiano kati ya nchi hizo mbili utaimarisha mfumo wa huduma za rufaa kwa wagunjwa watakaohitaji matibabu nchini Afrika Kusini.

"Kusainiwa kwa hati hii moja ya maazimio ya Mktano wa Pili wa mataifa mawili(Bi - National Commission - BNC) baina ya Tanzania na Afrika kusini ambapo Azimio Na. 43

lilielekeza kwamba, Hati ya Makubaliano katika sekta ya Afya isainiwe baada ya taratibu zote ambapo Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe Cyril Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini walisisitiza umuhimu wa kutekeleza maafikiano yaliyofikiwa na kutoa mrejesho wa utekelezaji kwa wakati" amefafanua Mhe. Ummy.

Kwa upande wake Mhe.Dkt. Phaahla amepongeza hatua ya kusainiwa kwa hati ya makubaliano haya ambayo imefanyika katika kipindi ambacho nchi za Dunia nzima na Bara la Afrika zikiwemo nchi za Afrika Kusini na Tanzania zinakabiliwa na majanga mbalimbali ikiwemo mababili ya tabia nchi inayopelekea milipuko ya magonjwa na ukosefu wa vyakula.



“Utaratibu wa Bima ya afya ni kuchangiana sio lazima mpaka uugue” – Dkt. Mollel

Na. Emmanuel Malegi
Dar es salaam

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amesema lengo la kuwepo na Mifuko ya Bima ya Afya ni wananchi kuchangiana gharama za matibabu kabla ya kuugua ili kuepusha familia hasa za masikini kwa kutumia fedha nyingi kugharamia matibabu.

Dkt. Mollel amesema hayo leo Septemba 25, 2023 jijini Dare Es Salaam wakati akiongea na Vyombo vya Habari ili kuelezea mafaniko ya Sekta ya Afya katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

“Katika kipindi cha awamu zote sita, Serikali imefanikiwa kuboresha Sekta ya Afya kwa ujumla, changamoto kubwa iliyobaki na inawayolikabili kundi kubwa la wananchi ni namna ya kuwawezesha kugharamia huduma za afya. Kwahiylo, ili kufikia dhama-ri ya Serikali ya Afya Bora kwa Wote ni lazima kama nchi kuwa na mfumo endelevu na imara wa uchangiaji wa gharama za matibabu kabla ya kuugua (Bima ya Afya)”. Amesema Dkt. Mollel.

Aidha, Dkt. Mollel amesema Mwaka 2016 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulianzisha mpango wa bima ya afya kwa

watoto walio chini ya miaka 18 (Toto Afya Kadi) kwa lengo la kuweshera kundi la watoto kwa ujumla wao kuijunga kupidia shule za awali, msingi na sekondari ili kun-ufaika na mpango huo

“Hata hivyo, pamoja na uhamasishaji uliofa-nyika kwa kupindi cha takriban miaka saba (7) bado mwitikio haukuwa wa kuridhisha kwani idadi ya watoto waliojiandikisha iliku-wa ni 210,000 kati ya lengo la watoto milioni 25 kwa kipindi hicho”. Amesema Dkt. Mollel

Dkt. Mollel ameongeza kuwa, kupidia uand-ikishaji wa kundi hilo, asilimia 99 ya watoto walioandikishwa walikuwa tayari na matati-zo ya kiafya ambapo kati ya takriban shilingi bilioni 5 zilizokusanywa kama michango yao, shilingi bilioni 40 zilitumika kugharamia matibabu hali iliyoenda kinyume na dhana na misingi ya uendeshaji wa mfumo wa bima ya afya.

Mwisho, ametoa rai kwa wananchi wote ambao bado hawajajiunga na utaratibu wa bima, wajunge sasa na pia pindi maamuzi yatakapofanyika ya kupidishwa kwa Bima ya Afya kwa wote wajitokeze kwa wingi kuijunga na Mfumo huu.





Tuongeze nguvu zaidi kupambana na Ugonjwa wa Kifua Kikuu ili tuutokomeze ifikapo 2030

Na. Englibert Kayombo,
New York USA.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ametoa rai kwa Jumuiya za Kimataifa kushirikiana na Serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa kuongeza nguvu zaidi ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kuweza kuutokomeza kabla ya Mwaka 2030.

Waziri Ummy amesema hayo leo alipokuwa akitoa tamko la Tanzania kuhusu mapambano dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kwenye vikao vinavyoendelea vya Mkutano Mkuu wa 78 wa Umoja wa Mataifa.

"Bado hakuna rasilimali za kutosha kupambana na TB, tunaendelea kuhimiza wadau wa Sekta ya Afya kuunganisha nguvu za pamoja na kuwekeza zaidi kwenye rasilimali, tafiti, teknolojia, vifaa na vifaatiba" amesema Waziri Ummy.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania ni mionganini mwa nchi 30 zenyet watu wengi wenye maambukizi ya Kifua Kikuu ikichangia asilimia 87 ya ugonjwa wa Kifua Kikuu duniani.

"Takwimu za mwaka 2021 zinaonyesha kuwa Tanzania ilikuwa na watu 132,000 wanaoqua ugonjwa wa kifua Kikuu, tumeweza kupunguza maambukizi mapya ya ugonjwa huu kwa asilimia 32 na vifo vitokanavyo na ugonjwa huo kwa asilimia 55" amesema Waziri Ummy na kusema kuwa Serikali inaendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kuutokomeza ifikapo 2030.

Katika kuhakikisha ugonjwa huo unatokomea ifikapo mwaka 2030, Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania imewekeza nguvu kubwa

kwenye utoaji wa matibabu ya Kifua Kikuu pamoja na utoaji wa elimu ya afya ili jamii iweze kufahamu ugonjwa huo mapema na kupata matibabu.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania inatekeleza Mpango Mkakati Shirikishi wa Sekta ya Afya katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu uliozinduliwa mwezi machi 2023 utakaosaidia kuongoza katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania inaungana na nchi nyinginezo chini ya Umoja wa Mataifa kwa kuendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa huo na imeridhia azimio lililokwa la kuendelea na mapambano dhidi ya Kifua Kikuu.



Serikali kushirikiana na Wadau kuimarisha Huduma za uchunguzi wa Maabara

**Na Said Nyaoza,
Dodoma**

Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kushirikiana na wadau wa huduma za uchunguzi wa magonjwa kwa kuimarisha huduma za uchunguzi wa maabara, Vifaa-Tiba, damu salama pamoja na ubora wa huduma ili kutekeleza maelekezo ya Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu.

Hayo ameyasema Mkurugenzi wa Huduma za Uchunguzi Dkt. Alex Magesa wakati akifungua mukutano wa kitengo cha huduma za uchunguzi wa magonjwa pamoja na wadau wa huduma za uchunguzi wa magonjwa kilichofanyika Jijini Dodoma.

"Tunaendelea kushirikiana na wadau hawa ili kuondoa kero kwa wananchi, ambapo mionganini mwa kero hizo ni pamoja na upatikanaji wa Vitendanishi, Vifaa, Vifaa-Tiba ikiwemo ya mionzi na upande wa damu salama", amesema Dkt. Magesa

Vile vile, Dkt. Magesa amesema mkazo unawekwa katika kuimarisha upatikanaji wa wataalamu wa maabara, radiolojia, na fundi sanifu vifaa tiba na kuwasilitiza wadau kutoa kipaumbele kwa ajira za muda mfupi kwa wataalamu wa kada husika.

Amesema, ili kufanikisha hayo lazima kazi ifanyike Kama timu ambapo kikao hicho kikimalizika wajumbe wataondoka na maazimio ambayo yatawezesha kwa kila mmoja kujua majukumu yake na anasaidiaje katika kufikia malengo makuu ya Wizara ya Afya na Serikali kwa ujumla.

"Lengo la mukutano huo ni kuwasiliana na kujadili vipaumbele vya huduma za uchunguzi wa magonjwa kwa wadau wote ili kuweka mikakati ya pamoja ya kufikia malengo ya Wizara ya Afya katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa". Amesema Dkt. Magesa.

Aidha, Dkt. Magesa amesema, Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alitoa malengo mbalimbali ambayo yanatakiwa kutekelezwa kwa wakati ili kutatua kero za wananchi ndio maana wameamua kuitisha nguvu ya pamoja ikiwemo nguvu za wadau.

Pia, amesema kwenye mashirikiano hayo yatawezesha kusongesha gurudumu la maendeleo katika upande wa uchunguzi na kutoa huduma zilizo bora ili kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.



Rasilimali zaidi zinahitajika kupambana na ugonjwa wa Malaria

**Na. Englibert Kayombo,
Newyork USA.**

Ili tuweze kuutokomeza ugonjwa wa malaria, tunahitaji rasilimali zaidi na uwajibikaji wenyewe kuleta matokeo chanya kwenye mapambano dhidi ya malaria.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu akiwa Jijini Newyork Marekani alipokuwa akiwasilisha taarifa ya mapambano dhidi ya Malaria kwa niaba ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango kwenye kikao cha kujadili ufadhili wa mapambano dhidi ya malaria Afrika kuitia Umoja wa Viongozi wa Afrika katika Mapambano dhidi ya Malaria (ALMA)

“Tunahitaji rasilimali zaidi kupambana na Malaria, ugonjwa huu unaathiri asilimia 1.3 ya ukuaji wa uchumi Barani Afrika ni lazima sasa tuwekeze zaidi na kuwajibika kwenye mapambano dhidi ya malaria kwa kushirikiana na wadau wengine” Amesema Waziri Ummy.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania inaendelea kuijimarisha kiuchumi kutokana na athari za janga la UVIKO-19 hivyo ni dhahiri kwamba rasilimali zinahitajika zaidi ili kuweza kufikia malengo ya kupambana na malaria.

Waziri Ummy amesema Tanzania inaendelea kuweka mkazo zaidi kwenye mapambano dhidi ya Malaria kwa kushirikiana na Sekta binafsi, Asasi za kiraia na Jamii kwa ujumla juu ya kukabiliana na ugonjwa wa Malaria.

“Tunashirikiana kwa ukaribu na Umoja wa Wabunge wanaopambana na Malaria pamoja na Magonjwa yasiyopewa Kipaumbele (TAPAMA) kuleta utashi wa kisiasa na ili wawe mabalozi wa kuelimisha na kuhamasisha zaidi jamii kwenye mapambano dhidi ya Malaria” Amesema Waziri Ummy.

Pamoja na hayo Waziri Ummy amebainisha kuwa Tanzania hivi karibuni imezindua Baraza la Kuto-komeza Malaria ambalo lina jukumu la kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali zaidi, kuelimisha jamii dhidi ya Ugonjwa huo ili kuongeza nguvu zaidi za mapambano dhidi ya Malaria.

“Tanzania, Afrika na Dunia nzima inaweza kuwa salama zaidi bila ya ugonjwa wa Malaria endapo kutakuwa na umoja kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huu” amesema Waziri Ummy Mwalimu.

Tanzania yahimiza usawa katika kukabiliana na Majanga

Na Englibert Kayombo,
Newyork USA.

Serikali ya Tanzania imelitaka Shirika la Umoja wa Mataifa la kuweka usawa kwenye kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na majanga yanayoendelea kutoka Duni-ani na kuziwesha nchi zinazoendelea kupata fursa sawa za uwekezaji wa viwanda vya dawa, chanjo, vifaa na vifaatiba, pamoja na misaada ya rasilimali kwenye kukabiliana na majanga.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu wakati akiwasilisha Tamko la Serikali kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kikao cha Azimio la Kukabiliana na majanga na dharura kilichofanyika kwenye Mkutano Mkuu wa 78 wa Umoja wa Mataifa Jijini Newyork.

Waziri Ummy amesema kuwa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania imejifunza mengi kuitia mlipuko wa Ugonjwa wa UVIKO-19 na namna ulivyoleta athari mbalimbali ndani ya jamii, hivyo sasa ni nyema kuwa na mikakati endelevu yenye usawa katika kukabiliana majanga.

"Kama nchi moja haipo salama, basi sote hatupo salama, tunahitaji kuona mabadi-liko ya usawa wa kupambana na majanga na kuwa na maazimio yenyе kuleta usawa kwenye mapambano dhidi ya magonjwa ya mlipuko na dharura za masuala ya afya" amesisigiza Waziri Ummy.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania ilipatwa na mlipuko wa ugonjwa wa Marburg mnamo mwezi wa tatu, na katika kipindi cha miezi 3 ilifanikisha mapambano dhidi ya ugonjwa huo ambao ultokea Mkoani Kagera.

!

Ametaja mkakati mojawapo wa kuongeza usalama wa masuala ya afya ni kupitia Watoa Huduma za Afya ngazi ya Jamii ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za afya ngazi ya msingi.





Vifaa vya kujipima UKIMWI Milioni 1.6 vimesambazwa Nchini

**Na. Shaban Juma,
Dodoma**

Wizara ya Afya kwa Kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI hadi sasa imeweza kusambaza vifaa vya mtu kujipima mwenyewe maambukizi ya Virusi vya UKIMWI zaidi ya Mil. 1.6 kuanzia Mwaka 2021 nchini Tanzania.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu leo kwenye kilele cha MdaHALO wa Kitaifa wa Baraza la Taifa la watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania (NACOPHA) uliofanyika kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma ambapo Mgeni rasmi alikua ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa.

Waziri Ummy amesema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI itaendelea kuongeza nguvu za kusambaza vifaa hivyo vya watu kujipima wenyewe Virusi vya UKIMWI ili kuweza kutambua hali zao wenyewe na kwa haraka kuhusu ugonjwa huo.

Waziri Ummy amebainisha kuwa Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeendelea kupanua wigo wa vituo vya kupima na kutoa huduma za matunzo (CTC) kwa watu wenye UKIMWI ambapo hadi sasa tuna vituo 8,529.

"Nitoe rai kwa watu wote wanaoishi na VVU kuzingatia matumizi sahihi na endelevu ya dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI ili kuweza kujilinda wao wenyewe lakini pia kuwalinda wengine" amesisitiza Waziri Ummy.

Pia, Waziri Ummy amesema Serikali kupitia Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI itaendelea kutoa huduma za kupima, tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU hapa nchini ili vituo vyote vinyo vya kupima na kutoa matunzo (CTC) kwa 95% ifikapo Mwaka 2025.

Aidha, Waziri Ummy amesema chini ya uongozi mahiri wa Rais Dkt. Samia, Serikali itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vitendanishi kwaajili ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na kuendelea kufuatilia taarifa zote kuhusu uwepo wa dawa mpya ambazo ni bora zaidi.

Wataalamu wa magonjwa ya Ini Afrika wakutana katika kongamano Tanzania

**Na. Shaban Juma
Dodoma**

Kongamano la Kimataifa la Sita la Magonjwa ya Ini Barani Afrika (COLDA) limezinduliwa jijini Dar es Salaam ambapo limekutanisha wataalamu wa magonjwa ya mfumo wa chakula na Ini, kutoka katika nchi 43 kwa lengo la kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu namna ya kukabiliana na kutibu magonjwa ya mfumo wa chakula na Ini.

Akizindua kongamano hilo kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mkurugenzi wa Tiba kutoka Wizara ya Afya Prof. Pascal Ruggajo amesema kuwa ni heshima kubwa kama nchi kuwa mwenyeji wa kongamano hilo kubwa ambalo limekutanisha wataalamu wa kada mbalimbali ikiwemo Wataalamu wa Uchunguzi, Radiolojia, Wapasuaji, Wataalamu wa Mionzi na dawa.

Prof. Ruggajo amesema Magonjwa ya ini barani Afrika na duniani kwa ujumla yanongezeka kwa kasi, ambapo Tanzania inakadiriwa kuwa kati ya watu 100 basi watu 4 Hadi 8 wana maambukizi ya homa ya Ini.

Prof. Ruggajo amesema Wizara ya afya inaandaa sera ya kukabili magonjwa mbalimbali inayojumisha Magonjwa ya VVU, Magonjwa ya ngono na Hepatitis B.

"Serikali imejipanga kukabiliana na magonjwa ya ini kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa vifaa vyta uchunguzi na tayari wataalamu kadhaa wa magonjwa ya homa ya ini wamepatiwa mafunzo nje ya nchi". Ameeleza Prof. Ruggajo.

Aidha, Prof. Ruggajo ametoa wito kwa wananchi kufanya uchunguzi wa magonjwa ya Ini na kupata chanjo.

Kwa Upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Prof. Mohamed Janabi amesema kuwa Hospitali hiyo ni kituo kimoja wapo cha kushughulikia matatizo ya ini na Mfumo wa Chakula kati ya vituo vinne vilivypo afrika, ambapo vituo vingine vipo Morocco, Misri na Afrika kusini na kwamba tayari kituo hicho kina wataalamu wenyewe weledi wa kutibu changamoto mbalimbali za magonjwa hayo.

Kongamano la COLDA linafanyika nchini kwa siku tatu ambapo awali lilitanguliwa na mafunzo ya kutibu magonjwa ya ini na mfumo wa chakula kwa kutumia matundu madogo.





Waziri Ummy asisitiza matumizi sahihi ya ARV kwa wenyewe VVU

**Na. Emmanuel Malegi,
Dodoma**


Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesitisitiza kuzingatia matumizi sahihi na endelevu ya dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI (ARV) kwa watu wanaoishi na Virusi hivyo ili kuendelea kujilinda na kuwalinda wengine.

Waziri Ummy ameyasema hayo Septemba 7, 2023 kwenye kilele cha Mdahalo wa Kitaifa wa Baraza la Taifa la watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania (NACOPHA) uliofanyika kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.

“Nataka kuwasitisitiza watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ni kuzingatia matumizi sahihi na Endelevu ya dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI ili kuweza kujilinda wao wenyewe lakini pia na kuwalinda wengine na ugonjwa huo”. Amesema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy amesema kuwa Jarida Maarufu la Kimataifa la Sayansi na Afya (Lancet) limethibitisha pasi na shaka ikiwa watu wenyewe Virusi vya UKIMWI wakitumia vizuri dawa za ARV basi inapunguza maambukizi kwa wengine kwa asilimia zaidi ya 70.

“Kwahiyo niwaombe sana ndugu zangu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI tuendelee kuzingatia matumizi sahihi na Endelevu ya dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI (ARV) ili tuwakinge na wenzetu”. Amesema Waziri Ummy



Watoto zaidi ya milioni 3 kupata chanjo ya Polio kwenye mikoa 6 nchini.

Na. Englibert Kayombo
Dodoma

Wizara ya Afya kwa kushirikiana Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wadau wa Sekta ya Afya inatarajia kuendesha Kampeni ya kutoa chanjo dhidi ya ugonjwa wa polio kwa watoto zaidi ya Milioni 3,250,598 walio chini ya miaka 8 kwenye Mkoa wa Rukwa, Kagera, Kigoma, Katavi, Songwe na Mbeya.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu Jijini Dodoma akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Kampeni ya chanjo dhidi ya ugonjwa wa Polio ambayo inatarajiwa kuanza kufanyika nchini kuanzia Septemba 21 hadi 24, 2023.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania inaendesha Kampeni hiyo ya chanjo kutokana na Wizara kupokea taarifa mnamo Mei 26, 2023 za uwepo wa mtoto mmoja mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi kumi na moja ambaye alionyesha dalili za kupooza kwa ghafla.

Mtoto huyo ambaye alitolewa taarifa kutoka Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa. Uchunguzi wa Maabara ulithibitisha kuwa mtoto huyu ana maambukizi ya virusi cha Polio.

“Napenda nichukue fursa hii kuwataarifu kuwa tutakuwa na Kampeni maalum ya utoaji wa chanjo ya matone dhidi ya Polio (nOPV2) kwa watoto wote wenyewe umri chini ya miaka nane (8). Kampeni hii itafanyika kwa siku nne (4) kuanzia tarehe 21 – 24 Septemba, 2023 katika Mikoa sita (6) inayopakana na nchi zenyenye mlipuko wa Polio.

“Lengo la kampeni hii ni kuwafikia watoto 3,250,598 waliozaliwa baada ya mwaka 2016 ili kuwakinga dhidi ya Kirusi cha Polio aina ya pili (Polio Virus Type 2) kinachoweza kusababisha ulemavu wa kudumu. Kwa Mkoa wa Rukwa tunatarajia kufikia watoto 391,883 Kagera 729,387 Kigoma 884,477 Mbeya 614,346 Katavi 227,862 na Songwe 402,643”. Amefafanua Waziri Ummy.

“Wakati wa Kampeni kutakuwa na watoa huduma za afya 5,291 kwa Mikoa yote sita (6) itakayofikiwa na zoezi hili ambapo kila timu itakuwa na watoa huduma watatu. Timu hizi zitakuwa zinatoa huduma ya chanjo kwa walengwa kuititia vituo vya kutolea huduma za afya, nyumba kwa nyumba, shulenii na maeneo mbalimbali ya mikusanyiko ikiwemo Nyumba za Ibada”. ameetelea Waziri Ummy.





Bima ya Afya kwa wote suluhu ya kudumu ya matibabu kwa rika zote

Na Said Nyaoza
Dodoma

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amesema, Bima ya afya kwa wote itakuwa suluhu ya kudumu kwa wananchi wote ikiwemo watoto wasio na wazazi na wasio-jiweza ambao awali walikuwa wakilipiwa na wahisani kupitia "Toto Afya Kadi".

Dkt. Mollel amebainisha hayo leo Septemba 8, 2023 wakati akijibu swali la Mhe. Abdul-Haffar Idrissa Juma Mbunge wa Mtoni katika Bunge la 12, kikao cha tisa, Jijini Dodoma

Dkt Mollel amesema ni kweli kuwa, mfumo wa kulipia watoto kupitia "Toto Afya Kadi" umebadilika na kwa sasa unafanyika kupitia utaratibu wa shule na vifurushi vy'a bima ya afya vy'a najali, wekeza na Timiza na kueleza suluhu ya kudumu ni kuingia kwenye Bima ya afya kwa wote itayotoa fursa kwa wananchi wote kupata matibabu bora katika vituo vyote.

"Suluhisho la kudumu ni kukamilika kwa Muswada wa sheria wa Bima ya

Afya kwa wote ambao tunaamini utawezesha watoto wengi zaidi wasio na walio na changamoto za kiafya ku-lipiwa Toto Afya Kadi". Amesema

Aidha, Dkt. Mollel amesema, Serikali imeendelea kutoa elimu mashulenii ili kutambua uwepo wa Bima ya afya kwa watoto, huku akitoa wito kwa wa-heshimiwa Wabunge kuendelea kutoa elimu kwa wananchi katika ngazi zote ikiwemo wazazi juu ya vifurushi vyenye matibabu kwa watoto na umuhimu wa Bima ya Afya kwa wote.

Pia Dkt. Mollel amesema, Serikali ina utaratibu wa kutoa matibabu bure kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharma za matibabu kupitia barua ya kiongozi katika eneo lake analoishi inayothibitisha hali yake ili apewe matibabu.



Watoa huduam 5,291 kutoa chanjo ya Polio

**Na Emmanuel Malegi
Dodoma**

Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu amesema katika kuendeleza mikakati ya kutoa chanjo dhidi ya Polio, wizara imeunda timu ya watoa huduma 5,291 waliopata mafunzo ya kutoa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Polio katika Mikoa sita nyumba kwa nyumba .

Prof. Nagu ameyasema hayo katika kikao cha waziri wa afya na waandishi wa Habari leo Jijini Dodoma akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Kampeni ya chanjo dhidi ya ugonjwa wa Polio ambayo inatarajiwa kuanza kufanyika nchini kuanzia Septemba 21 hadi 24, 2023.

"Wakati wa Kampeni kutakuwa na jumla ya timu yenye jumla ya watoa huduma za afya 5,291 kwa Mikoa sita (6) itakayofikiwa na zoezi hili ambapo kila timu itakuwa na watoa huduma watatu. Timu hizi zitakuwa zinatoa huduma ya chanjo kwa walengwa kuititia vituo vya kutolea huduma za afya, nyumba kwa nyumba, shulen na maeneo mbalimbali ya mikusanyiko ikiwemo Nyumba za Ibada". Amesema Prof. Nagu

Pia Prof. Nagu amesema wizara imeunda timu nzuri ambayo imepata mafunzo ya kutoa chanjo ili kuhakikisha watoto wote

wanafikiwa katika kupatiwa Chanjo dhidi ya ugonjwa wa Polio

Aidha Prof. Nagu ametoa rai kwa wazazi na walezi kutoa ushirikiano kwa watoa huduma za afya ili kuwezesha watoto wao kuchanjwa kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba.

"Tunawapa hamasa wazazi wahakikishe kwamba, wanawatoa watoto wao kupata chanjo hii ili kuwaepusha watoto wetu kupata ulemavu ambao kwakweli unakingika kwa kutumia chanjo". Ameongezea Prof. Nagu.





Wataalamu wa kutibu Saratani watakiwa kujikita katika kufanya tafiti

**Na. Emmanuel Malegi
Dar Es Salaam**

Wataalamu wa Magonjwa ya Saratani nchini wametakiwa kujikita katika kufanya tafiti za kisayansi zitazowezesha nchi kuwa na teknolojia na ubunifu utakaosaidia utoaji wa huduma hususani za saratani.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa Wizara ya Afya Prof. Pascal Ruggajo ambaye alimwakilisha Waziri wa Afya katika kongamano la pili la kisayansi la magonjwa ya Saratani linaloendelea jijini Dar es Salaam.

Prof. Ruggajo amesema kuwa kwa sasa tunahitaji majibu ya changamoto zetu yatokane na sisi wenyewe.

"Takwimu zinaonyesha kwamba wagonjwa wapya wa saratani elfu 40 hugundulika kila mwaka huku vifo vinavyohusishwa na saratani vikifikia elfu 27 kila mwaka hivyo ni dhahili tunahitaji kutafakari kwa kina na kuweka mikakati ya pamoja kama taifa" ameeleza Prof. Ruggajo

Amesema wakati wa tatizo la UVIKO-19 kila taifa lilijaribu kutumia rasilimali za ndani kuokoa watu wake hivyo ni muda umefika sasa wa tupate majibu ya kisayansi yatakayowezesha kuunda nyenzo na matumizi ya dawa

ikiwemo tiba asili za mwaafrika ambazo zinaonyesha kutoa matumaini katika matibabu ya saratani.

Aidha Prof. Ruggajo ameagiza kuwa bodi za kujadili wagonjwa wa saratani "Tumor Board" ziimarishwe na maamuzi ya bodi hizo yaheshimiwe kwa kuwa matibabu ya Saratani yanahuishisha kada zaidi ya moja

Kwa Upande wake rais wa chama cha Madaktari wa Saratani Tanzania (TOS) Dkt. Jerry Ndumbalo amesema kuwa mkutano wa pili wa wataalamu wa Saratani unalenga kuwaleta pamoja wataalamu mbalimbali wanaohusika kutibu saratani kutoka sehemu mbalimbali duniani ili kujadili jinsi ya kugundua saratani, kutibu kwa teknolojia mpya na kukinga.

"Mkutano huu umebeba kauli mbiu isemayo kuziba pengo katika utoaji wa huduma za saratani inayolenga kubainisha maeneo yenye upungufu katika utoaji wa huduma na kuyatafutia ufumbuzi" amesema Dkt. Ndumbalo

Endeleeni kumsaidia Dkt. Samia kulinda Afya za Watanzania - Mhe. Nyongo



**Na Majid Abdulkarim
Dar es Salaam**

Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI Mhe. Stanslaus Nyongo ametoa wito kwa mamlaka ya dawa na vifaa tiba nchini (TMDA) kuendeleza ufanisi walionao katika kuangalia ubora na usalama wa dawa na vifaa tiba ili kuzilinda afya za Watanzania.

Mhe. Nyongo ametoa wito huo leo Septemba 11, 2023 wakati ziara ya kamati ya kudumu ya Bunge ya afya na masuala ya UKIMWI ilipotembelea Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba ili kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka hiyo katika kuzilinda Afya za Watanzania.

"Sisi kama Wabunge, wawakilishi wa wananchi tunawategemea sana kwa usalama wa dawa zetu ambazo zinaenda kwa mwananchi ambae ndio mlaji wa dawa hizo". amesema Nyongo

" TMDA mnamlinda afya za watanzania, endeleeni na moyo huo, mnamsaidia Mhe. Rais katika kulinda jamii ya Watanzania kupitia usalama wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. " Amesema.

Baada ya ziara ya kukagua shughuli mbalimbali katika Mamlaka hiyo, Mhe. Nyongo ametoa rai kwa wananchi kuwa na imani na Mamlaka hiyo kwani inafanya kazi kubwa yenye ufanisi na inatambulika na Shirika la Afya Duniani kwa kupewa ithibati daraja la nne.

Aidha, Mhe. Nyongo amewataka wananchi kuendelea kutoa taarifa kwa vyombo husika ikiwemo TMDA kupitia *152*00# na kubofya namba 2 endapo watakutana na dawa ambazo sio salama na kuleta madhara katika jamii ili changamoto hiyo ishugulikiwe kwa haraka.

Sambamba na hilo, amewataka Serikali kupitia Wizara ya Afya kukaa na Wizara ya viwanda kuona namna ya kurejesha usalama wa chakula chini ya Wizara ya Afya kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba kwani ufanisi na ubora wa TMDA unaotambulika katika Shirika la afya Duniani utasaidia kwa kiwango kikubwa juu ya usalama wa chakula nchini.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amewapongeza Watumishi wa TMDA kwa jitihada kubwa katika utendaji unaosaidia usalama wa wananchi kupitia Dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Ameongeza kuwa, Wizara ya Afya inaendelea na makubaliano na Wizara ya viwanda ili kuona namna gani ya kurudisha Chakula chini ya Mamlaka ya dawa na vifaa tiba kulingana na utaratibu wa WHO..



Tunduma yapongezwa kwa kuajiri watumishi wa afya wa mkataba

Na Hassan Kimweri

Songwe

Waziri wa Afya Mhe.Ummy Mwalimu amewapongeza viongozi wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma kwa kuajiri watumishi wa Afya wa mkataba kwa kutumia mapato ya ndani.

Waziri Ummy ameyasema hayo Septemba 12, 2023 alipokuwa akizungumza na watumishi katika kituo cha Afya Tunduma wakati akiendeleza ziara yake ya siku Tatu katika Mkoa huo wa Songwe.

"Kipekee nimpongeze sana Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma pamoja na Mkurugenzi Mtendaji kwa kutumia mapato ya ndani kuajiri watumishi wa Afya wa Mkataba". Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy ametaka Halmashauri nyingine ziige mfano huo mzuri wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma kwa sababu fedha za mapato ya ndani zinakusanya kutoka kwa wananchi hivyo ni bora kutumia fedha hizo kutatua kero za wananchi.

Aidha, Waziri Ummy amesema upatikanaji wa dawa katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma upo vizuri ambapo dawa zinapatikana kwa asilimia 94.

"Asilimia 94 kubwa na nzuri lakini hizo asilimia Sita pia hatutaki kusikia dawa hakuna hasa katika awamu hii ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwakuwa anatoa fedha za dawa kwa 100%". Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy ametoa maelekezo kwa Mganga Mkuu wa Mkoa pamoja na timu yake kuhakikisha wanafanya kaguzi za mara kwa mara za kuangalia upatikanaji wa dawa.

"Hatutaki kusikia mtu anakosa dawa wakati fedha za dawa zipo, lakini kwa ujumla dawa zote muhimu zipo na hii ni kutokana na juhudzi za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuwajiali Watanzania". Amesema Waziri Ummy

Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Songwe ukamilike ndani ya miezi sita

Na Hassan Kimweri
Songwe

Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe ukamilike ndani ya miezi Sita hasa jengo la mama na mtoto, jengo la wagonjwa wa dharura (EMD) na jengo la wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu (ICU) ili wananchi wapate huduma haraka na kwa urahisi.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ameyasema hayo leo Septemba 13, 2023 alipokuwa anaongea na watumishi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe akiwa kwenye ziara yake ya kukagua utolewaji wa huduma, upatikanaji wa dawa pamoja na mradi wa ujenzi katika Hospitali hiyo.

“Fedha zimetolewa kwa nini ujenzi unachelewa, Sasa nataka ujenzi huu ukamilike hasa jengo la mama na mtoto, EMD na ICU ndani ya miezi Sita”. Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy amepongeza kukamilika kwa jengo la Maabara ambalo limekamilika kwa asilimia 100 na kuanza kufanya kazi katika Hospitali hiyo.

Aidha, Waziri Ummy amesema Hospitali zote za Rufaa za Mikoa ziwe na madaktari bingwa ili kusaidia huduma za kibingwa zinapohitaji katika Hospitali husika.

“Tutawapeleka madaktari bingwa katika kila Hospitali za Rufaa ya Mikoa ili waweze kusaidia huduma za kibingwa lakini pia madaktari wote watalipwa sawa na daktari aliyopo Muhimbili kwa kuwa wote ni sawa na wamesoma kitu kimoja”. Amesema Waziri Ummy





Wafamasia waelekezwa kuboresha namna ya uagizaji Dawa kulingana na uhitaji kwa jamii.

Na. Majid Abdulkarim
Dodoma

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amewaelekeza Wafamasia katika ngazi zote kuhakikisha wanaagiza dawa (maoteo) kulingana na aina ya magonjwa yanayoisumbua jamii yao pamoja na mzigo wa wagonjwa, ili kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa dawa kwa wananchi katika vituo vyta kutolea huduma.

Dkt. Mollel amesema hayo katika ziara ya kamati ya Bunge ya kudumu ya Afya na masuala ya UKIMWI ilipotembelea katika ofisi za Bohari ya Dawa Jijini Dar es Salaam ili kujionea shughuli mbalimbali za utendaji katika taasisi hiyo yenye majukumu ya ununuzi wa dawa, usambazaji pamoja na utengenezaji.

Ameendelea kwa kutoa wito kwa Wabunge kwa kushirikiana na madiwani katika majimbo yao kufuatilia kwa ukaribu masuala ya dawa katika vituo vyao vyta kutolea huduma za afya na kuhakikisha suala la dawa litakuwa ajenda ya kudumu katika vikao vyta Hal

mashauri kwani ndio yanayomgusa Mtanzania kwa karibu zaidi pindi anapoumwa.

Nae, Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) Bw. Mavere Tukai amesema, Bohari ya Dawa ipo kwenye utekelezaji wa mikakati iliyojiwekea ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa vituo vyote pamoja na ujenzi wa maghala mapya ikiwemo maghala mawili yanayojengwa Jijini Dodoma na Mtwara.

Ameendelea kusema kuwa, tayari MSD imewasilisha maombi ya fedha ili kukuza mtaji utaowasaidia kutoa huduma bora kwa vituo vyta kutolea huduma ili wananchi wanufaikia na huduma hizo.



Serikali kuendelea kuajiri watumishi wa Afya nchini

**Na. Hassan Kimweri
Songwe**

Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa Afya nchini kwa kuwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anatoa kibali cha kuajiri watumishi wapya katika Sekta ya Afya kila Mwaka.

Hayo ameyasema leo Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alipokuwa akizungumza na watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Mombasa wakati akiendeleza ziara yake ya siku Tatu katika Mkoa huo.



“Tunamshukuru sana Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kujali Sekta ya Afya ambapo anatoa kibali kila Mwaka cha ajira mpya Kwahiyo tutaendelea kuajiri lakini pia kutumia wadau wa maendeleo kuleta wataalamu hususan wa Maabara”. Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy amesema kufuatia changamoto hiyo ya uhaba wa watumishi katika Hospitali ya Wilaya ya Mombasa ni kutokana na kuongezeka kwa vituo vya Afya ambapo awali kulikua na vituo vya Afya Viwili na Sasa kuna Vituo vya Afya Vitano.

Aidha, Waziri Ummy amewataka watumishi wa Afya katika Hospitali ya Wilaya ya Mombasa kuhakikisha wanaendelea kufanya kazi kwa kufuata misingi ya Taaluma yao, weledi na maadili ili wananchi kuendelea kupata huduma bora.

“Muda wote tapohudumia wagonjwa tuzingatia weledi na Taaluma zetu na la pili tuzingatia maadili ya Taaluma yetu na la Tatu tuzingatia viapo vyetu kwa kuwa kazi yetu ni kuokoa maisha ya watu”. Amesema Waziri Ummy

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu yupo katika Mkoa wa Songwe kwa ziara ya siku Tatu kwa lengo la kukagua huduma zinazotolewa katika Hospitali a Wilaya, vituo vya Afya pamoja na Zahanati, pia upatikanaji wa dawa na utolewaji wa chanjo.

Wanahabari ni nguzo muhimu ya elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa wa Polio.

Na. Emmanuel Malegi,
dodoma

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule amewawaasa Waandishi wa Habari kuwa mabalozi katika utoaji wa elimu ya umuhimu wa Chanjo ya Matone dhidi ya Ugonjwa wa Polio kwani ni nguzo muhimu katika kuifikia jamii kwa haraka.

Senyamule amebainisha hayo leo Septemba 15 wakati akifungua Mafunzo kwa Waandishi wa Habari kutoka vyombo mbalimbali vya Habari vya Kitaifa na Mkoa wa Dodoma yenye lengo la kuwajengea uelewa kuhusu umuhimu wa kuandika Habari zenyetija katika uelemishaji juu ya ugonjwa wa Polio.

"Ninyi Wanahabari ni nguzo muhimu na mnaifikia jamii kwa uharaka hivyo nawaasa mkawe mabalozi katika kuelimisha jamii, nyie mkiamua mambo yafanikiwe inawezekana, mkiamua mambo yasifanikiwe inawezekana nichukue nafasi kuwapongeza". Amesema.

Aidha, RC Senyamule amewaomba viongozi wa mikoa husika kufuatilia zoezi la kampeni ya chanjo litakapofanyika ili kufanya kwa ufanisi huku akitoa wito kwa wananchi kuendelea kuwapeleka watoto kupatiwa chanjo.

Akitoa mafunzo kwa wanahabari Meneja Mpango wa Taifa wa Chanjo Florian Tinuga amesema lengo la mafunzo hayo kwa wanahabari ni kuwezesha kupata elimu kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa Polio na kuwezesha kupata uelewa juu ya kinga zake.

Aidha, Dkt. Tinuga amesema mionganini mwa dalili za ugonjwa wa Polio ni pamoja na kulemaa kwa ghafla, kulegea kwa kiungo, kukosa nguvu, kushindwa kunyanya mguu au mkono, mtoto kushindwa kukaa ambapo amesisitiza mtu yeyote aonapo dalili kama hizo ni muhimu kuhakikisha mtoto anapelekwa kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kilicho karibu.

Halikadhalika ametoa ujumbe kwa jamii kuendelea kuimarisha usafi, kunawa mikono mara kwa mara pamoja na kuendelea kuchukua tahadhari ili kujilinda na ugonjwa hatari wa Polio kwani unasababisha kupooza au ulemavu wa kudumu na hatimaye kifo.

Ikumbukwe kuwa kamjeni ya chanjo ya Matone dhidi ya Ugonjwa wa Polio inatarajiwa kuanza Septemba 21-24, 2023 katika Hal-mashauri 37 kutoka mikoa 6 ya Kigoma, Kagera, Mbeya, Songwe, Katavi na Rukwa na walengwa ni watoto walio na umri chini ya miaka minane na wanatarajiwa kufikiwa watoto takriban Milioni 3.25.



RMO's waagizwa kukamilisha maandalizi ya chanjo Polio

Na Shaban Juma
Songwe

Waganga Wakuu wa Mikoa ya Rukwa, Songwe, Katavi, Mbeya, Kigoma na Kagera wametakiwa kukamilisha maandalizi ya kampeni ya Kitaifa ya chanjo dhidi ya ugonjwa wa Polio inayotarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 21 hadi 24 Septemba 2023 katika Mikoa hiyo ili kuwaongezea kinga watoto.

Kauli hiyo imetolewa leo na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu alipofanya kikao na watumishi wa Sekta ya Afya Mkoani Rukwa baada ya kukagua maandalizi ya utoaji wa huduma ya chanjo ya polio.

"Niwaelekeze waganga wote wa Mikoa itakayota chanjo wafanye maandalizi kabla ya tarehe ya zoezi la chanjo, muhakkishe kwenye vituo vyote vya utoaji chanjo kuna kila kitu kinachohusiana na chanjo na watoa chanjo wapiti nyumba hadi nyumba". Amesema Prof. Nagu.

Aidha, Prof Nagu amewataka Waganga Wakuu wa Mikoa kuhakikisha wanatoa hamasa kwa wananchi kupitia viongozi wa

kidini, watu mashuhuri katika Jamii na kwa kupitia vyombo vya habari na kurasa za mitandao ya kijamii.

Pia, Prof. Nagu ameendelea kusitiza kufikiwa kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka Nane pasipo kujali changamoto za kijiografia kwani mikakati iliyowekwa kupitia huduma tembezi ni kuhakikisha chanjo hiyo inawafikia watoto wote wanaoishi katika maeneo ya mbali na maeneo yasiyofikika kwa urahisi kwa kuwa na timu zitakazotoa huduma hiyo.

Hata hivyo, Prof. Nagu amesema kutokana na ugonjwa wa Polio huambukiza kupitia kinyesi hivyo amewataka wananchi wote wakumbushwe na kuelekezwa juu ya kudumisha usafi na matumizi sahihi ya vyoo.

Mwisho, Prof. Nagu ameyashukuru mashirika ya kimataifa, likiwemo Shirika la Afya Duniani (WHO) na UNICEF, kwa ushirikiano wanaoendelea kuutoa kwa Serikali ya Tanzania katika kutokomeza magonjwa ya mlipuko ikiwemo ugonjwa wa Polio



Wizara ya Afya kufanya tathmini baada ya kukabiliana na Uviko-19

**Na Cletus Sanga
Dar es Salaam**

Baada ya miaka Minne ya kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19, Wizara ya Afya imechukua jukumu la kufanya zoezi la tathmini kwa namna ilivyokabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo nchini.

Hayo yamesemwa leo na Mfamasia Mkuu wa Serikali Bw. Daudi Msasi wakati akifungua kikao cha Kwanza kwa zoezi hilo la tathmini kwa niaba ya katibu Mkuu Wizara ya Afya.

“Wizara imeona ni wakati sahihi kufanya tathmini hiyo na kwa mujibu wa kanuni za udhibiti wa magonjwa ya mlipuko ni vizuri kufanya tathmini ili kuimarishe namna ya kukabiliana na magonjwa kama

hayo kwa nyakati za usoni”. Amesema Bw. Msasi

Amesema, lengo ni kuainisha masuala yaliyofanyika vizuri, kubaini changamoto na mapungufu katika mapambano ya UVIKO-19, na namna ya kuweza kukabiliana na matukio kama hayo endapo yatajitokeza kwa nyakati zijazo.

Aidha, Bw. Msasi amewataka washiriki wote kwenye kikao hicho cha tathmini kuwa huru katika kutoa taarifa sahihi na maoni yao kwa kuwa kikao hicho hakina lengo la kumlaumu yeyote wala kunyosheana vidole bali kimelenga zaidi kufanya tathmini na kuboresha njia nzuri zaidi za kuweza kukabiliana na majanga kama ya UVIKO-19 endapo yatajitokeza tena nchini.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Dharura na Maafa Wizara ya Afya Dkt. Angela Samwel amesema tathmini hiyo baada ya kukabiliana na mlipuko wa UVIKO-19 imehusisha wadau mbalimbali kutoka Wizara, Taasisi za Serikali, Waganga Wakuu wa Mikoa, Hospital za Serikali na Binafsi na wengine kutoka Mashirika ya Umoja wa Mataifa na wadau wa maendeleo.

Dkt. Angela amesema taarifa ya tathimini hiyo itahusisha masuala mazuri yaliyofanyika wakati wa kukabiliana na UVIKO-19, Changamoto na Mapungufu pia itapendekeza hatua za muda mfupi na muda mrefu za kuchukua ili kuendeleza masuala mazuri na kuboresha mapungufu yaliyojitokeza na itawasilishwa kwa viongozi na wadau mbalimbali.





Bilioni 5.9 zimetumika kununua viuadudu katika Halmashauri nchini

**Na.Majid Abdulkarim,
Dodoma**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imetumia kiasi cha shilingi Bilioni 5.9 kununua viuadudu katika ngazi ya Halmashauri ndani ya kipindi cha mwaka 2017 hadi 2023.

Hayo yamebainishwa leo Bungeni Jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel wakati akijibu maswali ya Wabunge katika kikao cha Bunge la 12.

Dkt. Mollel amesema ili kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa viuadudu kutoka kiwanda cha Kibaha kwa kipindi cha mwaka 2024-2026, Wizara ya Afya imeomba kupatiwa jumla ya Shilingi Bilioni 129.1 kwa ajili ya utekelezaji wa afua ya unyonyiziaji wa viuadudu ili kuangamiza viluilui wa mbu kwenye mazalia ili kufikia lengo la kutokomeza malaria ifikapo 2030.

"Wizara ya Afya inashirikiana na Shirika la Taifa la Maendeleo ya Viwanda kuhakikisha Kiwanda kina-pata ithibati kutoka Shirika la Afya Duniani ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha za kutekeleza wa afua hii kutoka kwa wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria". Ameeleza Dkt. Mollel.

Aidha, Dkt. Mollel amesema Serikali chini ya uongozi imara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, immeendelea kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali zote ili kutatua changamoto ya dawa nchini.

Katika kutatua changamoto ya dawa nchini Dkt. Mollel amesema serikali imeanza utekelezaji wa kuipatia mtaji Bohari ya Dawa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ili kuwa na bidhaa za Afya muda wote.

Ameongeza kuwa Serikali imetoa fedha za ununuzi wa bidhaa za afya kila mwezi kwa ajili ya vituo vyatolea huduma za Afya vya Umma ili kukabiliana na upungufu wa dawa.

Hali kadhalika, Dkt. Mollel amesema Serikali itahakikisha suala la usimamizi wa bidhaa za afya linakuwa sehemu ya ajenda ya Kudumu ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa pamoja na kusimamia watoa huduma katika vituo vyatolea huduma za afya ili kuweza kukadiria kwa usahihi (Forecasting).

"Vituo vyatolea huduma za afya kutumia fedha zinazotokana na malipo ya huduma na dawa kununua bidhaa za afya kuliko kutegemea fedha zinazotolewa na Serikali pekee pia itasaidia kutatua changamoto ya upungufu wa dawa



Waandishi wa habari wajengewa uwezo juu ya ugonjwa wa Sikoseli

Na Shaban Juma
Dodoma

Wizara ya Afya kupitia Idara ya Tiba imetua mafunzo ya ugonjwa wa Sikoseli kwa waandishi wa Habari Mkoa wa Dodoma zaidi ya vyombo 40 kwa ajili ya kuwajengea uwezo ili waweze kupata uelewa na kuweza kusaidia kutoa elimu kwa wananchi juu ya ugonjwa huo.

Hayo ameyasema leo Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Wizara ya Afya Dkt. Caroline Damian wakati akifungua semina kwa waandishi wa habari juu ya ugonjwa wa Sikoseli iliyofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Afya Jijini Dodoma.

“Mwezi wa Tisa ulimwenguni kote tunazimisha mwezi wa uelewa wa Sikoseli kwa jamii, hivyo tumeanza kutoa elimu kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Dodoma zaidi ya vyombo 40 ili waweze kusaidia kuielimisha Jamii juu ya ugonjwa huo”. Amesema Dkt. Caroline

Aidha, Dkt. Caroline amesema kuwa mchango wa waandishi wa habari ni mkubwa sana Katika kuwafikia wananchi hivyo wataweza kuwafikia Watanzania wengi zaidi kwa kuwapa elimu juu ugonjwa huo wa Sikoseli ili kupunguza tatizo hili hapa nchini.

“Tunaamini kwamba waandishi wakielewa vizuri watakuwa kwenye nafasi nzuri ya kujibu maswali na kutoa elimu kwa Jamii ya kutosha”. Amesema Dkt. Caroline

Pia, Dkt. Caroline amesema kuwa kuna dhana potofu nyingi katika jamii kuhusiana na ugonjwa wa Sikoseli kwa sababu ni ugonjwa wa kurithi hivyo waandishi wa habari ni kundi muhimu sana litakaloweza kwenda kutoa elimu kwa jamii waondokane na dhana potofu hiyo.

Hata hivyo Dkt. Caroline ameiasa Jamii kupata elimu sahihi juu ya ugonjwa huo wa Sikoseli ambapo itawawezesha wasimamia Sera ya Afya kuweza kuwapata Watoto waliopo kwenye Jamii wenye ugonjwa huo ili waweze kupatikana matibabu sahihi.

“Jamii ikipata uelewa vizuri ambao ni sahihi itawezesha kuondokana na dhana potofu ambapo inapelekea wengine kuwaficha watoto wao hivyo itasaidia kupatikana kwa watoto wenye tatizo hilo na kuwapatia tiba sahihi sababu ukiwa na ugonjwa wa Sikoseli unaouwezekano mkubwa wa kupona”. Amesema Dkt. Caroline

Tanzania kufikia lengo la Afya kwa wote mwaka 2030.



Na Englibert Kayombo New York USA.

Serikali ya Tanzania imejidhatiti kutekeleza malengo ya kufikisha huduma za afya kwa wote hadi ifikapo mwaka 2030.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu jana akiwa kwenye kikao cha Huduma za Afya kwa wote kilichofanyika kwenye Mkutano Mkuu wa 78 wa Umoja wa Mataifa Jijini Newyork.

"Tanzania inaungana na wajumbe wengine wa kikao hiki katika kutekeleza azimio hili la kuhakikisha kila mwananchi anafikiwa huduma bora za afya popote alipo". Amesema Waziri Ummy Mwalimu.

Waziri Ummy amesema kuwa upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi nchini Tanzania zimeendelea kuimarike kutoka asilimia 38 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 43 mwaka 2022 huku bajeti ya afya ikiendelea kuboreshwa maradufu kutoka Dola Milioni 529 mwaka 2019 hadi kufikia Dola Milioni 950 mwaka 2022.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania imendelea kutekeleza azimio la Afya kwa wote waliloweka Viongozi wakuu wa nchi kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa

mwaka 2019 kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wote, kuhamashisha wananchi kuijunga na skimu mbalimbali za Bima ya Afya.

"Serikali ya Tanzania inaendelea kutenaga fedha kuhakikisha inafikia lengo la afya kwa wote ikiwemo kuwasilisha muswada wa bima ya afya kwa wote katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". Amesema Waziri Ummy.

Amesitisiza ili kufikia lengo la afya kwa wote ni lazima huduma za afya ngazi ya msingi ziboreshwe ili wananchi waweze kupata huduma bora za afya wakiwa karibu zaidi na maeneo yao, kuimarisha utoaji wa elimu ya afya pamoja na kuongeza nguvu za mapambano dhidi ya magonjwa na utoaji tiba.

"Tunahimiza ushirikiano wa pamoja kati ya Serikali na wadau wa sekta ya afya kuungana pamoja katika kufikia malengo tuliyoweka ya afya kwa wote hadi ifikapo mwaka 2030 kwa kuwekeza kwenye Ubunifu wa Teknolojia mpya, Rasilimali, mbinu bora za kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza pamoja na Huduma za chanjo na dawa". Amesisitiza Waziri Ummy

Serikali imewe ka kipaumbele cha kuwalinda watumishi wa afya katika kupambana na magonjwa ya mlipuko na magonjwa hatarishi

**Na. Englibert Kayombo,
Dodoma**

Waziri wa Afya Mh. Ummy Mwalimu amesema kipaumbele cha kwanza cha Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kupambana na magonjwa hatarishi na magonjwa ya mlipuko kwa kuwalinda watumishi wa afya.

Waziri Ummy amesema hayo akiongozea majibu ya swali la nyongeza liloulizwa na Mheshimiwa Jackline Ngonyani Msongozi (Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma) bungeni kuhusu kuwalinda watumishi wa afya katika kutoa huduma kwa wagonjwa wa magonjwa ya mlipuko.

"Rais Samia Suluhu Hassan anatuwezesha kwa kutoa vifaa kinga vya kutosha kwa ajili ya watumishi wa afya, pale kunakotokea changamoto yoyote kwa mtumishi wa afya wakati wa kutoa Huduma serikali inafanya kila linalowezekana kuokoa maisha ya mtumishi huyo". Amesema Waziri Ummy.


Ameeleza kuwa kabla ya mtumishi wa afya kuanza kuhudumia mgonjwa wa magonjwa hatarishi na ya mlipuko anapewa mafunzo ya jinsi gani ya kuhudumia wagonjwa wa magonjwa hayo.

Akitoa mfano wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa Marburg Mkoani Kagera amesema kuna mtumishi alipata changamoto ya kupata maambukizi lakini serikali ilifanya jitihada za kupeleka madaktari Bingwa saba na wauguzi bingwa pamoja na kupeleka mashine ya kusafisha figo kwa lengo la kuokoa maisha.

Aidha, Waziri Ummy amewashukuru watumishi wa afya na kuwatia moyo kwa kuendelea kutoa Huduma za afya kwa watanzania.



Tanzania ina jumla ya Madaktari Bingwa wazalendo 2,469



**Na Majid Abdulkarim
Dodoma**

Tanzania ina jumla ya Madaktari Bingwa Wazalendo 2,469 ambao wamesajiliwa na Baraza la Madaktari Tanganyika wa fani mbalimbali za Uadtari Bingwa.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel wakati akijibu swal namba 103 la Mhe. Angelina Adamu Malembeka (VITI MAALUM) aliyeuliza Tanzania ina Madaktari Bingwa Wazalendo wa magonjwa ya Binadamu wangapi na katika magonjwa gani, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu bungeni leo Jijini Dodoma

Mhe. Godwin Mollel amesema kuwa kati yao Madaktari Bingwa 2,098 wapo katika Sekta ya Umma na Madaktari Bingwa 371 wapo Sekta Binafsi.

Amesema madaktari hao wamegawanyika katika maeneo 28 ya Ubingwa kwa lengo la kutoa Huduma kwa wananchi.

Dkt. Mollel akijibu swal namba 104 kutoka kwa Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi aliyeuliza lini Serikali itatoa fidia kwa Madaktari na Manesi wanaopoteza maisha wakihudumia Wagonjwa wa Magonjwa ya Mlipuko ambapo amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

inatambua na kujali mchango mkubwa wa Watumishi wanaohudumia wagonjwa wa magonjwa ya milipuko wakiwemo madaktari na wauguzi.

"Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba Serikali hutoa fidia kwa watumishi waliofariki kwa sababu za kuwahudumia wagonjwa wa magonjwa ya mlipuko kwa Sheria ya Fidia kwa wafanyakazi Sura ya 263 marejeo ya Mwaka 2015 kupitia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Tanzania". Ameeleza Dkt. Mollel .

Ameeleza kuwa fidia zinazotolewa kwa mtumishi wa afya wakati anapopata changamoto ni pamoja na gharama za mazishi na pensheni kwa wategemezi wake.

Hata hivyo amewapongeza watumishi wa afya kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa huduma za afya kwa wananchi ili kuhakikisha taifa linakuwa salama



Tufanye kazi kwa ushirikiano ili kuboresha huduma za afya nchini.

**Na Hassan Kimweri,
Dodoma**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amewata-ka watendaji ndani ya Sekta ya Afya kufanya kazi kwa ushirikiano na kuleta tija katika kuboresha ubora wa huduma za afya nchini.

Waziri Ummy amesema hayo leo Septemba 5, 2023 alipokuwa akizungumza na Menejimenti ya Watumishi wa Wizara ya Afya kuhusu mipango ya utekelezaji wa afua za kufikia vipaumbele 14 ambavyo vimewekwa na Wizara ya Afya kwenye Bajeti ya mwaka 2023/24.

"Dhamira yangu ni kuboresha ubora wa huduma za afya nchini, tufanye kazi kwa ushirikiano na kuweka mbele maslahi ya Sekta ya Afya na Tanzania," amesema Waziri Ummy.

Pia, Waziri Ummy amesitiza watendaji ndani ya Sekta ya Afya kuijua vyema Sekta na kufanya mambo yenye tija katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Amesema kuwa, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa katika kuboresha Sekta ya Afya nchini kwa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za Afya, ununuzi wa dawa, vifaa na vifaatiba, ajira za watumishi pamoja na kusomesha wataalam, hivyo ni wajibu wa watendaji ndani ya Sekta ya Afya kuhakikisha wanaboresha huduma za afya wanazotoa kwa wananchi.

"Sekta ya Afya ina fedha nyingi na wadau wengi wanaofanya kazi, naomba tuelekeze fedha hizo katika kuboresha huduma za Afya ili wananchi waweze kunufaika na upatikanaji wa huduma bora za Afya", amesitiza Waziri Ummy.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu amesitiza watendaji ndani ya Wizara na Sekta ya Afya kwa ujumla kufanya kazi kwa umoja na kushirikiana katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Dkt. Jingu amesema kuwa watendaji wana dhama kubwa ya kutatua kero za wananchi hivyo ushirikiano wa karibu katika kuhudumia wananchi utaleta tija katika uboreshaji wa huduma za Afya nchini.





Tujikinge dhidi ya Kichaa cha Mbwa

Na. Cletus Sanga, Dodoma

Wananchi wametakiwa kuwachanja wanyama wanaowafuga ili kujikinga na kupambana na ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkoo, Bw. Arbogast Waryoba, wakati wa maadhimisho ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa duniani yaliyofanya Wilaya ya Mpwapwa Mkoani Dodoma.

Aidha Waryoba amesitiza kuwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa unaathiri afya ya mtu kutokana na kuambukizwa na kirusi kitokanacho na wanyama jamii ya Paka, Mbwa, Mbweha, Fisi ambapo huambukizwa kwa kung'atwa na mnyama wenye ugonjwa huo.

"Pamoja na ugonjwa huu kusababisha vifo, ugonjwa huu umesababisha athari za kiumumi kwa sababu ya garama ya matibabu yake. Ugonjwa huu unakadirwa kusababisha vifo 59,000 duniani". Amesema Waryoba

Aidha Waryoba amesema kuwa serikali imeendelea kutekeleza juhudzi za kudhibiti ugonjwa huu kwa kutoa elimu kwa umma, kuboresha utekelezaji wa dhana ya afya nchini, kurahisisha upatikanaji wa chanjo ya Kichaa cha Mbwa kwa wananchi, na chanjo kwa wanyama, hasa mbwa na paka,

Sambamba na hilo Waryoba amesema kuwa serikali inaendelea kutekeleza juhudzi za kudhibiti na kupambana na ugonjwa huu kwa kuangalia namna ya kupunguza bei ya chanjo kwa wanyama.

Hata hivyo Waryoba amesema serikali imewezeshwa na shirika la usambazaji wa chanjo duniani kuridhia chanjo ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa kuingizwa katika mfumo wa chanjo za kawaida, ambazo garama zinatarajiwa kushuka zaidi pale taratibu za utekelezaji wa jambo hili utakapokamilika.

Aidha amesema kuwa katika kipindi hiki cha maadhimisho, jumla ya dozi 180,000 za chanjo ya Kichaa cha Mbwa zimesambazwa nchini kuanzia Septemba 24 mpaka 28, ambapo jumla ya mbwa 9,500 na paka 150 wamekwisha chanja.

Hata hivyo, juhudzi za pamoja zinahitajika kwa sekta zinazohusika ili kuutokomeza ugonjwa huu. Kutokana na madhara ya ugonjwa huu kwani serikali imechukua jukumu la uchanjaji wa wanyama hao ikiwa ni sehemu ya upambanaji dhidi ya ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa.

LILI YA RUFAA KANDA YA KUSINI MTWA



Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI SEPTEMBERA, 2023

